# Nitakuwa na furaha kama... nitakuwa na ujasiri wa kugawanya!

"Heri masikini wa roho maana ufalme wa mbinguni ni wao" (Mt. 5,3)

## Lengo

Kujifunza kutoa na kupokea kwa kupima mahitaji yako na yale ya wengine.

## Mambo yaliendaje?

Mwanzoni kuna sehemu ya makaribisho, ambapo inabidi kuacha nafasi ya mazungumzo na mawasilisho ya kile ambacho kila mtu ameishi, mangámuzi na magumu pia. Kukaribisha maana yake ni kumfanya kila mtu ajisikie nyumbani: ubunifu utatusaidia kupata mbinu zinazofaa. Pia tunaweza kujikumbusha malengo tuliyojiwekea kwenye mkutano wa mwisho: "ulikuwaje?"

## Shughuli ya utambulisho

**Maono ya video na tafakari**

**"NGUVU YA UKARIMU"** (AMBATISHO)



**MUDA:** videoclip 3'05'' pamoja na tafakari ni kama dakika 30

**VUFAA:** vifaa ili kuona kipande cha video, kalamu na karatasi kwa kila kikundi, ramani ya mji

**UENDESHAJI:** kabla ya kutazama kipande cha video inashauriwa kufanya tafakuri, (brain storming)katika makundi madogo ya watu (3/4), juu ya dhana ya "ukarimu". Kila kikundi, kikifikiri juu ya mang' amuzi ya matukio ya ukarimu ya mtu binafsi au ya wengine, kinakubaliana juu ya ufafanuzi na kutafuta tabia tatu muhimu za ukarimu (mfano. Wa bure, wa wote, wenye kuzaa, nk). Halafu makundi yanabadilishana matokeo na mang'amuzi yoyote yaliyojitokeza kutokana na kazi ya kikundi.

**MAPENDEKEZO:** Video inaonesha maisha ya mtu mkarimu na kufungua suala la ukarimu wa kurudishiana: "Anapata nini mtu aliye tayari kugawanya alichonacho?" Ili kundi lipate kutafakari inawezekana kusimamisha video katika dakika ya 1'49 " na kufungua mjadala juu ya kile anachopata mhusika aliye kwenye video kutokana na huu mtindo wa maisha. Maono ya mwisho yatathibitisha au kutothibitisha utabiri wa kundi.

**HITIMISHO:** Mwishoni kundi linaweza kutaja "Maeneo" ya ukarimu katika mji wake, na kuchora ramani ya mji. Ni pointi ambazo kwazo fadhila hii inawekwa katika matendo na inaweza kuimarishwa na wanamji na pia na vijana wa kundi.

## Tuishi hivi

Yote yalianza jioni moja wakati, tulipokutana na baadhi ya gen3 katika familia moja iliyokuwa na matatizo makubwa ya kiuchumi, tuligundua kwamba hawakuwa na jiko. Tulipotoka nje tuliambiana: “hatutajipa amani mpaka tutakapopata jiko.” Mmoja wetu alikuwa na jiko lisilotumika katika karakana yake ambalo mama yake alifurahi kulitoa. Tukajitosa katika foleni ya Palermo ili kulipeleka mara moja. Kando yetu vijana wengi walikuwa wanaharakisha kwenda kwenye burudani za Jumamosi jioni. Kwetu hakuna kitu kilichoweza kutupatia furaha kuliko kukimbia na kwenda kumpa mtu furaha. Kutokana na mang’amuzi haya lilizaliwa wazo la tendo endelelvu: operesheni ‘mfuko’. Tulitoa mifuko mitupu ya kufanyia manunuzi kwa marafiki na ndugu, tukawaomba waturudishie hiyo mifuko ikiwa na vyakula ambavyo tutawapelekea wahitaji. Baada ya wiki moja mifuko ilirudishwa ikiwa imejaa kabisa. Tangu hapo operesheni inarudiwa kwa mafanikio. tuliona nyuma mifuko imejazana. Katika usambazaji tunatatizo la uchaguzi, kwa kuwa orodha ya familia za kusaidia inaongezeka.

*(Palermo – Italia)*



## Kwangu ilitokea...

Kwa undani

## KUTOA, UCHAGUZI NI WETU



***Vera Araujo (mwanasosholojia),*** *Utamadunin wa kutoa – Kongamano kuu 2002 – Warsha ya vijana - Loppiano, 28 Mei 2002.*

### Unaweza kutwambia juu ya utamaduni wa kutoa?

Tunaweza kusema kuwa kuna tamaduni mbili,... namna mbili za kuona na kuelewa maisha: kwa upande mmoja ubinafsi ambapo kila mtu anatafuta maslahi yake, starehe zake, (...), utamaduni unaotokana na huu ubinafsi ni ule ambao sisi twaweza kuuita 'utamaduni wa kupata'. Kupata, kutaka vitu kunatawala mtindo wa maisha wa watu wengi na wa vijana wengi, uchaguzi wao umeelekezwa katika ulaji, kwa ile tamaa isiyozuilika ya kumiliki vitu. Je, mnajua matokeo yake? Bila hata kujitambua, tunakuwa watu wa fujo, tunakuwa watu wa vurugu, tunakuwa wahusika wakuu wa malumbano na migongano katika maisha ya kijamii, kwa sababu kila mtu anajifikiria yeye mwenyewe tu. Na tunakuwa wahusika wakuu wa vita kati ya watu, vita zinazuka kutokana na ubinafsi. Hii ni aina ya utamaduni: utamaduni wa kupata.

Likini si huo tu, sisi tunaweza kuwa wahusika wakuu wa utamaduni mwingine, utamaduni uliotofauti na ule wa kupata, huu ni tamaduni wa mtu mpya, wa vijana wapya, wasio na ubinafsi, ambao si wamiliki tena bali watoaji. Na huu utamaduni mwingine ni utamaduni wa kutoa. (...) lakini tunapokabiliana na huu utamaduni ili kuuishi, ili tuufanye kuwa wetu, ni lazima tujiulize swali: tunatoa kwa jinsi gani? Ni kwa namna gani tunapaswa kutoa? Angalieni, 'kutoa' si kitu rahisi, si tendo jepesi, ni sanaa, kuna mtindo wake, kuna namna yake ya kuenenda, hivyo ni lazima tuelewe, tujifunze sifa za kutoa, ili tuweze kutoa vizuri, kwa sababu kutoa haitoshi, ni lazima kutoa vizuri.

Basi sifa ya kwanza ya kutoa ni haki, ni lazima kutoa bure. Kutoa ni tendo lisilo na kutarajia, kwa maana ya mtu akitoa ili apate, huko si kutoa kwa kweli, mtu akitoa kwa ubatili,... ili wengine waone kuwa ametoa, huko si kutoa kwa kweli. Kutoa ni kwa bure, hii ni sifa ya kwanza.

Sifa nyingine ya kutoa ni furaha, ni lazima kutoa kwa furaha, kwa furaha kamili. Kuna neno la Yesu kwenye Injili linalosema: «kuna furaha zaidi katika kutoa kuliko katika kupokea». Mama Teresa wa Calcutta, tuzo kwa ajili ya amani, alisema: «Anayetoa kwa furaha, anatoa vizuri, anayetoa kwa furaha, anatoa zaidi, Mungu humpenda anayetoa kwa furaha. Kuna furaha ya ndani katika kutoa kwa sababu kile tunachopokea ni kikubwa zaidi ya kile tunachotoa». Hivyo, furaha, ukamilifu wa furaha ni sifa nyingine ya kutoa.

Na mwisho, sifa ya tatu ya kutoa ni wingi, kutoa kwa wingi, siyo kuhesabu. (...) hata hapa kunasentensi moja nzuri ya Mama Teresa wa Calcutta iliyokuwa inasema: «kitu kimoja nawasihi,

msiogope kutoa, lakini msitoe kilicho cha ziada, toeni hata kile kinachowagharimu, sitaki mnipatie mabaki, nataka mnipatie kile mnachojinyima». (…)

Lakini tunaweza kuuliza swali jingine: ni nini tunapaswa kutoa? Kwanza kabisa mali za kiroho ambazo ni za muhimu zaidi. Zawadi ya kwanza tunayopaswa kuwapa wengine ni zawadi ya sisi wenyewe, ya upendo wetu, ya urafiki wetu, zawadi ya amani, ya kukaribisha, ya kusikiliza, zawadi ya sisi, zawadi za kiroho. Siku moja Chiara alitwambia: «tuna utajiri mwingi tunaoweza kuuweka shirika hata kama hauonekani, kwa sababu mtu anaweza kusema: "lakini mimi sina kitu"». Badala yake Chiara anasema: «Mna utajiri mwingi. Kwa mfano tuna nguvu za kimwili na za kiakili, tuna upendo moyoni wa kutoa, tuna urafiki wa kudhihirisha, tunafuraha ya kushirikisha, tuna muda wa kuwapa wengine, tuna sala zetu, utajiri wa ndani wa kuweka shirika kwa sauti au kwa maandishi. Wakati mwingine tuna hata vitu halisi: mabegi, peni, vitabu, hela, vitu vya kutoa ».


Huu utamaduni wa kutoa, tukiuishi, utajenga ndani yetu mantiki mpya, namna mpya ya kufikiri na ya kuona vitu na kutufanya tuwe na uwezo wa kuushinda utamaduni wa kupata hata kwa matendo, utatufanya tuweze kupambana na tamaa ya kumiliki na kuwa na kiu ya madaraka. Utatufanya hasa tuwe na uwezo wa kujenga jamii ambapo kuna kugawana, ushirika wa vitu kati ya wote ili kuufikia ushirika wa umoja wa nyoyo. Tunaweza kujenga dunia mpya pale ambapo vijana pamoja na watu wazima ni wahusika kwa sababu ni wajenzi, si watazamaji tu, bali wajenzi. Tunaweza kusema kuwa kwa huu utamaduni wa kutoa, dunia mpya inawezekana.

## NILIMCHAGUA MUNGU TU



*Chiara Lubich,*
*Neno la uzima,*
*Julai 1979*

(…) tulikuwa tunamwita Eletto. Alikuwa kijana mrefu, mzuri, mwenye akili na tajiri. Aliposikia sauti ya Mungu ili amfuate, hakufikiri hata kidogo. Hakurudi nyuma. Kwake ni kama utajiri haukuwepo. Alitoa kila kitu. Alipokuwa anafanya tendo la upendo kwa ajili ya mvulana mmoja alifariki akiwa na miaka 33 tu. Pale, kuna ubao ulioandikwa haya maneno yake: «Nilimchagua Mungu tu, si kitu kingine». Eletto, alipofika mbele ya Yesu, bila shaka hakujisikia kurudia maneno: "Ni rahisi kwa ngamia kupita katika tundu la sindano, kuliko tajiri kuingia katika ufale wa Mbingu" (Mt. 19,24) (…)yanamguso fulani haya maneno ya Yesu? Tujaribu kuelewa maana halisi ya haya maneno ya Yesu. Yesu hazihukumu mali zenyewe, bali si tajiri anayezing'ang'ania. Kwa sababu vyote ni mali ya Mungu na tajiri anafanya kama vile utajiri ni wake. Ni mtazamao gani inabidi awe nao mtu aliye na mali? Inabidi awe na moyo ulio huru, ulio wazi kabisa kwa Mungu, ajisikie kuwa ni msimamizi wa mali zake. Mali za dunia hii, kwa kuwa si mbaya, hakuna haja ya kuzidharau, lakini inabidi kuzitumia vizuri. Si mkono bali moyo inabidi uwe mbali nazo. Ni kujua jinsi ya kutumia kwa ajili ya manufaa ya wengine.



## Nitajaribu!

Chiara aliwapa gen 3 jukumu la kueneza utamaduni wa kutoa kwa vijana wengine. Mtaenezaje utamaduni huu kwa Chipkizi wa Umoja wa mji wenu? Waulizeni viongozi na wahamasishaji wa Chipkizi wa Umoja halafu andaeni tukio la kufanya pamoja na chipkizi wa mji wenu. Baadaye mtapata mbinu bora za KUGAWANA chemchemi ya furaha:

1. Kutengeneza furushi, au kuangalia kama kati ya vitu tulivyonavyo hakuna vya ziada ambavyo vinaweza kuwafaa wengine. Kusambaza kwa wanaohitaji vitu tulivyovikusanya kutoka kwenye jumuiya.
2. Kuchagua familia moja, rafiki aliye katika shida wa kumsaidia.
3. Je, tunahitaji watu wengine wajiunge nasi, Vijana na watu wazima? Katika maeneo mengine ulifunguliwa ukurasa wa Face Book (FB) wa binafsi ambapo kila mtu anashirikisha anachotaka au anasema hitaji lake au la mtu mwingine anayemjua.

## Tupo katika hatua gani?

*Ili **kulifikia lengo** ni lazima kufanya mazoezi kila siku na kutambua mabadiliko mazuri na magumu yaliyojitokeza. Itatusaidia hadi katika mkutano ujao, tutakapotenga muda wa kushirikishana mang'amuzi.*

Nilifaulu kuishi kwa matendo utamaduni wa kutoa?

Na nani?

Niligawa nini?

Kitu gani kimebadilika ndani yangu na kando yangu?

**Kwa ajili ya mlezi**

## Tathmini baada ya mkutano

- Shughuli zilizopendekezwa zilikuza mvuto wa vijana kwa hii heri?
- Kuna eneo la pekee lililojitokeza ambalo gen 3 wanaona kuwa ni vigumu kutekeleza umasikini wa roho?
- Walichukua dhamira gani ili kuiishi? Lengo liwe kuwaongoza na kuwasaidia katika pendekezo lao hadi mkutano ujao.
- Nafikiri kuwa mada imekamilika au nadhani kuwa kuna kitu kinachokosekana cha kukijadili katika mkutano ujao?
- Kuna magumu yaliyojitokeza? Ni kitu gani cha muhimu kukumbuka ili kuboresha wakati ujao?